

# Kwa nini mtoto wangu apate chanjo ya COVID-19?

Chanjo hii husaidia kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa ugonjwa wa Korona. Chanjo hii inakinga jamii kwa kupunguza kuenea kwa COVID-19.



## Je, watoto kweli wanahitaji chanjo hii ya COVID-19 kwa sasa?

Ndio. Hatari ya kuambukizwa COVID-19 bado iko juu. Kadiri watoto wanavyopokea chanjo haraka, ndivyo wanavyojikinga zaidi.



## Je, mtoto wangu wa miaka 5-11 atapokea chanjo gani ya COVID?

Watoto walio na miaka 5-11 nchini Canada watapokea dozi ndogo cha chanjo ya Pfizer-BioNtech (Mikrogramu 10, theluthi moja ya kipimo kinachotumiwa kwa vijana na watu wazima). Dozi ndogo hufanya kazi vizuri kwa watoto wa sababu wao wana mfumo wa kinga ulio imara kuliko watu wazima. Watahitaji kupokea dozi mbili.



## Je, chanjo ya COVID-19 ni salama kwa watoto?

Idara ya Afya nchini Canada, wanasayansi kadhaa na watafiti wamechunguza kwa makini ushahidi wa kimatibabu uliopo na hawana wasiwasi wowote kuhusu usalama wa chanjo hii. Madhara ya kawaida zaidi ya chanjo hii ya COVID-19 ni sawa na madhara madogo yanayotokana na chanjo nyinginezo, kama vile maumivu katika sehemu iliyochomwa sindano, uchovu, maumivu ya mwili, maumivu ya kichwa, homa na homa ya baridi. Madhara haya hutoweka baada ya siku chache.

Kwa nadra sana, baadhi ya vijana na watu wazima walipata uvimbe wa misuli ya moyo (hali inayojulikana kama myocarditis) au uvimbe wa bitana ya nje ya moyo (hali inayojulikana kama pericarditis) baada ya kupokea chanjo ya COVID-19; wengi walipata nafuu baada ya siku chache. Katika tafiti za watoto wa miaka 5-11 ambao walipokea chanjo ya COVID-19, hakuna aliyepata uvimbe wa moyo. Kuugua COVID kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha uvimbe wa moyo kuliko chanjo yenyewe.

**Chanjo ya COVID-19 inaweza kuwasaidia watoto kudumisha afya ili wabaki shuleni na waweze kukaa na marafiki. Hakikisha mwanao amechanjwa haraka iwezekanavyo!**

Toleo hili linaanza kutumika 3 Desemba, 2021

{ REFUGEE } 613

BEHIND GOOD HEALTH  
**TAIBU**  
COMMUNITY  
HEALTH CENTRE

Funded by:

Financé par :



Immigration, Refugees  
and Citizenship Canada

Immigration, Réfugiés  
et Citoyenneté Canada

**OCASI**  
Ontario Council of Agencies Serving Immigrants

**WCHH**  
WOMEN'S COLLEGE HOSPITAL  
Healthcare | REVOLUTIONIZED